**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Uchunguzi wa Changamoto za Walimu na Wanafunzi wa Kiswahili katika Shule za Upili Nchini Kenya

*Linnah Apondi Okeyo[1*] Prof. John N. Kimemia, PhD na Dkt. Sophia M. Ndethiu, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100. Nairobi, Kenya
[*] Barua pepe ya mawasiliano: okeyo.linnah@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*26 Oktoba 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Changamoto, Visababishi, Mikakati, Ufunzaji na Ujifunzaji, Mwelekeo mseto, Kiswahili na Matokeo.*

**IKISIRI**

Lengo la utafiti ni kuchunguza changamoto walizokabiliana nazo walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika shule za upili nchini. Kiswahili ni lugha rasmi na ya taifa nchini Kenya tena ni somo la lazima linalofundishwa na kutahiniwa katika shule za msingi na za upili. Kimataifa, ni lugha inayotambuliwa kama chombo cha mawasiliano. Kuimudu lugha hubainika kupitia ujuzi wa mtu katika stadi zake kuu; kusoma, kuandika, kusikiliza, na kuongea. Umilisi na utendaji katika lugha hata hivyo huweza kuathiriwa pakubwa na mambo kadhaa. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Utabia na Utambuzi. Muundo wa utafiti ulikuwa usoroveya na ulinganishi, vifaa vilivyotumiwa kukusanya data vilikuwa hojaji, mahojiano, mtihani wa insha na uchunguzi darasani. Sampuli lengwa ilifikiwa kwa kutumia usampulishaji maksuudi na nasibu. Data ilichanganuliwa kitakwimu kwa kutumia uchanganuzi wa tarakimu na maelezo. Utafiti huu uligundua kuwa wanafunzi pamoja na walimu walipata shida kadhaa hali iliyoathiri kwa njia hasi ufunzaji na ujifunzaji wao. Licha ya kutambua umuhimu wa mwelekeo mseto katika ufunzaji, walimu wengi hawakutumia mbinu hii kufunza kutokana na ukosefu wa vifaa na nyenzo za kufunzia, uhaba wa muda, idadi kubwa ya wanafunzi madarasani mwao, uhaba wa walimu pamoja na ukosefu wa ujuzi maalum katika mbinu mseto. Pana haja kuu walimu waelekezwe vilivyo katika mbinu mwafaka za kufunzia, wanafunzi wahamasishwe kuhusu umuhimu wa somo hili, wachapishaji kuelekezwa vilivyo katika maswala yanayofunzwa katika kila kiwango na ukaguzi wa kina kufanywa ili kuondoa mambo yanayoweza kuwakanganya walimu na wanafunzi. Utafiti zaidi unaweza kufanywa katika vipengele vya Lugha na Fasihi ya Kiswahili ili kutambua changamoto zinazoshuhudiwa katika ufunzaji wao ili kuzitatua ipasaavyo.

**APA CITATION**

Okeyo, L. A., Kimemia, J. N. & Ndethiu, S. M. (2023). Uchunguzi wa Changamoto za Walimu na Wanafunzi wa Kiswahili katika Shule za Upili Nchini Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 412-434. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**CHICAGO CITATION**

Okeyo, Linnah Apondi, John N. Kimemia and Sophia M. Ndethiu. 2023. “Uchunguzi wa Changamoto za Walimu na Wanafunzi wa Kiswahili katika Shule za Upili Nchini Kenya”. *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 412-434. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538.

**HARVARD CITATION**

Okeyo, L. A., Kimemia, J. N. & Ndethiu, S. M. (2023) “Uchunguzi wa Changamoto za Walimu na Wanafunzi wa Kiswahili katika Shule za Upili Nchini Kenya”, *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 412-434. doi: 10.37284/jammk.6.1.1538.

**IEEE CITATION**

L. A. Okeyo, J. N. Kimemia & S. M. Ndethiu “Uchunguzi wa Changamoto za Walimu na Wanafunzi wa Kiswahili katika Shule za Upili Nchini Kenya”, *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 412-434, Oct. 2023.

**MLA CITATION**

Okeyo, Linnah Apondi, John N. Kimemia & Sophia M. Ndethiu. “Uchunguzi wa Changamoto za Walimu na Wanafunzi wa Kiswahili katika Shule za Upili Nchini Kenya”. *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Oct. 2023, pp. 412-434, doi:10.37284/jammk.6.1.1538.

## UTANGULIZI

Tatizo la wanafunzi kutofanya vyema katika mtihani wa Kiswahili limekuwepo na limekuwa likiwasumbua na kuwakosesha usingizi wengi. Mikakati ya kuimarisha matokeo haya imewekwa na washikadau mbalimbali lakini bado matokeo haya hayaridhishi (Kimani, 2015). Hii ina maana kuwa bado kuna mambo ambayo yanastahili kuzingatiwa ili kujaribu kuboresha hali ilivyo sasa. Mtafiti alipata kichocheo cha kutafiti kuhusu jinsi ya kuimarisha matokeo ya Kiswahili katika shule za upili hasa katika kaunti za Kisumu na Kakamega kwa kuzingatia changamoto za walimu na wanafunzi katika shughuli za ufunzaji na ujifunzaji wake. Mfumo wa elimu wa 8-4-4 huhitaji kuwa mwalimu afunze Lugha ya Kiswahili na Fasihi akitumia mbinu mseto. Kwa kuwa walimu hawakupewa mafunzo maalum kuhusu ufunzaji kupitia mbinu hii, wengi wao huitumia katika viwango tofauti tofauti kulingana na uwezo wao wa kuifasiri. Kwa hivyo, palikuwa na haja ya kuimarisha uwezo na maarifa ya mwalimu ya kutumia mbinu mseto afunzapo. Kwa mujibu wa Ng’ong’a (2002) kusetwa kwa mtaala kuna changamoto tele.

Kulingana na Ogott na Odera (2012) ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili unaweza kufaulu vyema kupitia hali ya kusetwa kwa vyombo vya habari na vifaa vya kidigitali. Gathumbi na Ssebbunga (2005) wanabainisha kuwa vifaa vizuri vya kufunzia lugha huwa na sifa zifuatazo; huegemea sana upande wa mwanafunzi, huibua ubunifu wa wanafunzi, huchochea uwezo wa kufanya kazi au zoezi, inapendeza na kulingana na hali halisi ya maisha au shughuli za kawaida. Vifaa vya ufunzaji ni muhimu katika kufaulisha ufunzaji na ujifunzaji japo matumizi ya vifaa hivyo kiholela hayawezi kufanikisha ufunzaji bora au hata mawasiliano kamilifu. Hivyo basi, ni jukumu la mwalimu kuhakikisha kuwa ameviteua vilivyo na kuvitumia kikamilifu ili kufanikisha juhudi za ufunzaji na ujifunzaji.

Gudu (2015) asisitiza kuwa kuna jambo tatanishi nchini kutokana na hali kuwa wengi wa wanafunzi wanaohitimu somo la shule ya sekondari hawana uwezo mkuuwa kuwasiliana kikamilifu na kuonyesha umilisi wao wa lugha ya Kiswahili katika maongezi yao na mara nyingi wao huchanganya ndimi au hata hutumia Kiingereza badala ya kutumia Kiswahili sanifu. Mfumo wa elimu wa 8-4-4 umeathiri pakubwa ufunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kuwa mtaala wake umekuwa mpana zaidi. Mtaala hautoi muda wa kutosha kwa wanafunzi kupata nafasi ya kutosha ya kufanya mazoezi katika matumizi ya lugha hii kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi madarasani, viwango vya chini vya umilisi na utendaji wa wanafunzi pamoja na changamoto zao za kitamaduni (Al-Hosni, 2014; Alharbi, 2015). Hatimaye, walimu huendelea kutumia mbinu za jadi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

katika ufunzaji ili waweze kukamilisha mada zinazolengwa kwenye silabasi hiyo kiwakati (Lumala, 2007; Njagi na wengine, 2014). Kutokana na shida za wanafunzi wanaohitimu masomo ya shule ya sekondari kutoweza kutumia lugha vilivyo, pana haja ya kuuangazia tena utaratibu wa kufunza Kiswahili katika shule za upili nchini. Ni wazi kuwa hali hii imesababishwa na mitindo ya utahini nchini ambayo haiangazii stadi zakusikiliza na kuzungumza katika mitihani ya kitaifa na hali zilizomo darasani zinazozuia mazoezi ya maongezi kufanywa kwa wingi pamoja na ukosefu au uhaba wa nafasi za kutosha nje ya darasa zinazoweza kutumiwa kufanyia lugha hiyo mazoezi ya kutosha (Alharbi, 2015).

**Suala la Utafiti**

Kwa kipindi kirefu sasa, tatizo la wanafunzi kutofanya vyema katika mtihani wa Kiswahili limekuwepo na limekuwa likiwasumbua na kuwakosesha usingizi wengi. Tatizo la utafiti huu lilikuwa ni kubaini masuala yanayochangia katika matokeo haya duni kwa lengo la kuimarisha matokeo hayo. Ni kutokana na hali hii ndipo mtafiti alipata kichocheo cha kutafiti kuhusu changamoto zilizowakumba walimu na wanafunzi wao katika shule za upili hasa katika kaunti za Kisumu na Kakamega kwa kuzingatia visababishi vyao, mikakati ya kuzikabili na hatimaye athari zao kupitia matokeo ya ufunzaji na ujifunzaji wenyewe

**Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni mahususi yafuatayo;

- Kueleza mambo ambayo husababisha mielekeo/mitazamo ya walimu na wanafunzi katika Kaunti za Kisumu na Kakamega kuhusu lugha, mbinu na mazingira ya kufunza na kujifunza Kiswahili.
- Kutambulisha namna ambavyo changamoto hizi pamoja na mikakati inayotumiwa huathiri shughuli ya ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na matokeo yake kwa jumla.

## NADHARIA YA UTAFITI

Utafiti huu ulielekezwa na mihimili ya nadharia mbili tofauti; mtazamo wa utambuzi ulioasisiwa na Gestalt mnamo 1920 na ule wa kitabia ulioasisiwa na Skinner na Pavlov mnamo 1904 – 1990. Nadharia zilizoeleza ujifunzaji kama vile nadharia ya utambuzi ya Gestalt ilisisitiza uhusishaji wa wanafunzi kikamilifu kwa kuwa kumsikiliza tu mwalimu afunzapo, wanafunzi hupokea na kuhifadhi asilimia kumi pekee (10%) lakini wanafunzi wanapohusishwa katika maongezi na matendo, wao hupokea na kuhifadhi asilimia themanini (80%) ya waliyofunzwa (Aggarwal, 2001). Katika utaratibu wa kumhusisha mwanafunzi katika ufunzaji na ujifunzaji darasani, wanafunzi wanahitajika kujiundia mawazo, mielekeo na kutawala ujifunzaji wao. Jukumu la mwalimu huwa tu ni kujenga mazingira mwafaka, kuwapa changamoto zilizostahili kukabiliwa kulingana na uwezo wao pamoja na mazoezi ya kielimu yaliyowasaidia kuibua maarifa yaliyofaa huku wakipata ujuzi wa kujenga misingi yao katika stadi mbalimbali pamoja na thamani. Utafiti huu ulitegemea nadharia hii ili kuchunguza iwapo walimu na wanafunzi walishirikiana vilivyo katika ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa kufuata mtazamo wake. Kwa hakika, kufunza huwepo ikiwa kuna hali ya kupokea na kumudu tabia geni.

Kulingana na Skinner kiwango kifaacho cha ujifunzaji huwepo tu iwapo kuna hali ya kubadilisha tabia ya mwanafunzi (Dewald, 1999). Kwa wafuasi wa nadharia ya tabia, ujifunzaji hutokana na utazamaji wa utamaduni unaopatikana katika mazingira (Plotkin, 2003). Ili matendo fulani yatendeke lazima kuwe na vichocheo ambavyo huweza kuwa chanya kwa kutuza au hasi kwa kuadhibu (Baumgartner na wengine, 2003). Utafiti ulionyesha kuwa mikakati ya wafuasi wa nadharia ya tabia ya uimarishaji kupitia tuzo ni njia mwafaka kabisa katika uundaji wa tabia chanya katika

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

mazingira yoyote ya ujifunzaji. Mikakati hii huathiri mafanikio ya wanafunzi kwa njia chanya (Dawning na wengine, 2005).

Kwa mujibu wa wafuasi wa nadharia ya tabia, tabia za waja lazima zidhibitiwe (Liu na Mathew 2005) kwa kuwa kwao, mja ni kama mashine inayoweza kuwashwa na kuzimwa (Birzer, (2003). Nadharia hizi hivyo basi zilifaa katika kuelekeza utafiti huu kwa kuwa ile ya utambuzi ilimwongoza mtafiti kuelewa kuwa mitazamo hutokana na yaliyohifadhiwa akilini mwa kila mtu na kwa kuwa akili huelekeza tunayoyatenda. Pia, nadharia ya tabia ingezingatiwa katika hatua hiyo hasa kupitia uchunguzi wa darasani, kuchunguza matendo ya walimu na wanafunzi madarasani kupitia uteuzi wa na matumizi ya mbinu na vfaa vya kufunzia na kujifunzia.Mtazamo wa utambuzi ulisaidia katika kuelewa kwamba kila mwanafunzi hujifunza kwa njia ya kipekee kutegemea vifaa na mbinu maalum inayotumika kufunza. Mtazamo wa kitabia ulilenga sana tabia za walimu na wanafunzi darasani na jinsi ambavyo tabia hizo ziliundwa na kukuzwa kutokana na mielekeo yao na ilivyoathiri hali na shughuli za kufunza na kujifunza somo la Kiswahili.

## MBINU ZA UTAFITI

### Sampuli Lengwa ya Utafiti

Utafiti ulihusisha shule 24; 12 katika kaunti ya Kisumu na 12 Kisumu. Stadi za usampulishaji zilizotumiwa katika uteuzi wa sampuli ya utafiti zilikuwa nasibu na utabakishaji makusudi wa shule za aina tatu; shule za umma za wasichana, wavulana na za mseto. Shule nnenne katika kila kategoria ziliteuliwa na kuhusishwa katika utafiti. Baada ya uteuzi wa shule, walimu na wakuu wa idara katika shule hizo walihusishwa katika utafiti pamoja na wanafunzi wa kidato cha tatu kimaksuudi na kinasibu katika shule zenye mikondo mingi. Kerlinger (1978) anasema kuwa mbinu ya nasibu humpa mtafitiwa nafasi ya kuteuliwa kwa ajili ya uchunguzi darasani. Walimu na wanafunzi walijaza hojaji mbalimbali, walishirikishwa katika uchunguzi darasani huku wanafunzi wakifanya mtihani wa insha ya kiubunifu na wakuu wa idara wakihojiwa.

### Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti huu ulikuwa wa usoroveya na ulinganishi. Kupitia majibu ya wasailiwa katika hojaji zao pamoja na uchunguzi darasani mtafiti aliweza kutambua changamoto zilizowakabili walimu na wanafunzi wao katika ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Utafiti huu ulishughulikia uchunguzi wa mambo yaliyoathiri ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili, visababishi vyao, mikakati iliyotumiwa ili kuyakabili vilivyo pamoja na athari zao katika shughuli nzima ya ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Utafiti huu ulikuwa wa utaratibu wa ulinganishi kwa kuwa mtafiti alitaka kulinganisha na kubainisha tofauti au mlingano uliopo kati ya shule za Kakamega na Kisumu.

### Uchanganuzi na uwasilishaji wa Matokeo

Data ilichanganuliwa kitakwimu kwa kutumia uchanganuzi wa tarakimu na maelezo na kuwasilishwa kwa njia ya chati, jedwali na nukuu za wasailiwa mbalimbali..

## MATOKEO


### Changamoto za Wanafunzi

Utafiti ulichunguza changamoto ambazo wanafunzi walikumbana nazo walipofunzwa na kujifunza Kiswahili. Matokeo yalidhihirisha kuwa walikuwa na changamoto mbalimbali. Rejelea kielelezo hiki;

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

**Chati 1: Maoni ya Wanafunzi kuhusu Changamoto zao Shuleni**




Wanafunzi wengi walipokuwa shuleni walikabiliana na shida tatu kuu zilizokuwa kelele, uhaba wa vifaa na ukosefu wa muda wa kujifunzia. Maoni haya yanawiana na ya Kimani (2015), Mlay (2010), Earthman (2004) na Muruguru (2000). Earthman anaelezea kuwa kiwango cha juu ya kelele, hali ya joto na hewa huweza kuathiri ujifunzaji wa L2. Hii inaelezea kwa nini wanafunzi walikosa kufanya vyema katika somo la Kiswahili katika kaunti zote; Kisumu na Kakamega. Muruguru alisisitiza kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya uwepo wa vitabu ambavyo ni nyenzo muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji na utendaji katika somo la lugha. Kimani aligunda kuwa kulikuwa na uhaba wa baadhi ya vifaa vya kufundisha Kiswahili na kwingineko havikutumika. Mlay aligundua kuwa changamoto za ukosefu wa muda wa kutosha wa kudurusu, kelele, kutomotishika kudurusu pamoja na vikwazo vingine kama uhaba au ukosefu wa misaada kutoka kwa wazazi huathiri matokeo kwa namna hasi kwani husababisha matokeo ya wanafunzi kuwa duni. Chanagmoto hizi ziliathiri kwa njia hasi ufunzaji na ujifunzaji hivyo kusababisha matokeo ya wanafunzi katika somo kuwa duni.

## Maoni ya Wakuu wa Idara kuhusu Changamoto za Wanafunzi

Changamoto zilizotajwa zaidi na wakuu wa idara Kisumu zilikuwa za uzembe wa wanafunzi, kutojiamini na kutowaendea walimu ili waelekezwe. Katika kata ya Kakamega, uzembe, mielekeo hasi na kutojiamini ndizo zilizotawala. Shida ya uhaba wa vifaa na vitabu ilishamiri sana Kisumu huku ukosefu wa muda ukitajwa sana Kakamega. Matokeo haya yanalingana na madai ya Onyango (2008) kuwa wanafunzi wengi walikuwa wazembe; uzembe wao ndio uliowafanya wafanye makosa katika L2. Uzembe huo hata hivyo uliweza kusababishwa na mbinu za ufundishaji na pia vifaa anavyotumia mwalimu kufundishia. Kutojiamini kuliwaathiri wanafunzi katika ujifunzaji wao kama ilivyobainika katika mtihani wa Insha ya kiubunifu walioandika; kuliathiri matokeo yao kwa njia hasi. Pia, yanaingiliana na maoni ya Munawaroh (2017) aliyebainisha kuwa iwapo wanafunzi hawana ushirikiano mzuri na walimu wao, wao huzembea masomoni hivyo hukosa motisha ya kujifunza na hatimaye hukosa kuelewa wala kumudu wanaofunzwa. Fauka ya hayo,matokeo haya yanalingana na yale ya Mlay (2010) aliyegundua kuwa uzembe ulionekana kutamalaki miongoni mwa wanafunzi wengi jambo lililohuzunisha sana kwani liliathiri ufunzaji na ujifunzaji wao. Wanafunzi hawa hawakuwaendea walimu ili waelekezwe kwa kuwa walikosa uhusiano mzuri nao, wengi wao walidhihirisha kuwa walimu wao waliwatisha (kuwatia hofu) walipowafunza kwani walikuwa wakali jambo lililofanya wengine wao kutaka wabadilishiwe walimu.


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

Matokeo haya yanaonyesha kuwa wanafunzi walipata muda wa kutosha wa kudurusu na vifaa vya kujifunzia kwa kiasi,uhaba huu uliweza kuathiri kwa njia hasi shughuli ya ufunzaji na ujifunzaji wao madhali hawakufanya vyema katika mtihani wa insha ya Uamilifu walioiandika. Madai haya ni sawa na yale ya Munawaroh (2017) aliposisitiza kuwa vifaa vya kufundishia vya kutosha vikiwemo shughuli ya ufunzaji na ujifunzaji hufanikishwa vyema japo vikiwa vichache au hata kukosekana kabisa ufunzaji na ujifunzaji hutatizika pakubwa. Isitoshe, yanaoana na maoni ya Ogero (2012) na Kang'ahi na wengine (2012) kuwa matokeo duni katika mtihani wa Kiswahili huweza kusababishwa na mambo kama mbinu na vifaa vya kufunzia, kutotenga muda wa kutosha wa kudurusu mada za Kiswahili pamoja na uhaba wa vifaa vya kufunzia Kiswahili.

Kutowaendea walimu ili waelekezwe kulisababishwa na hali kuwa wanafunzi walikosa uhusiano mzuri na walimu wao kwa kuwa wengi wao walidhihirisha kuwa walimu wao waliwatisha (kuwatia hofu) walipowafunza kwani walikuwa wakali jambo lililofanya wengine wao kutaka wabadilishiwe walimu. Matokeo haya ni sawa na ya Kobia na Ndiga (2013) waliogundua kuwa wanafunzi wengi (asilimia 77.6) hawakuwaendea walimu wao walipokuwa huru bali wachache wao (asilimia 22.6) waliwaendea ili waelekezwe.

**Chati 2: Changamoto za wanafunzi; maoni ya wakuu wa Idara**




Changamoto nyinginezo zilitambuliwa kuwemo kama vile changamoto ya lugha nyinginezo katika umilisi wa lugha ya Kiswahili. Chambilecho mkuu mmoja wa idara Kakamega (mashambani):


> *"Athari ya lugha ya mama na sheng' huvuruga ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwani wanafunzi waliozoea lugha hizo huathirika kimatamshi, kisarufi na kimsamiati. Wao huishia kuchanganya na kubadili msimbo katika mawasiliano yao yote; kimaandishi na kimaongezi"* (MK 15).

Matokeo haya yanawiana na ya Ogero (2012), aliyetambua mambo yanayoweza kuchangia matokeo ya wanafunzi kuwa duni katika somo la Kiswahili kuwa, athari za lugha kama sheng' na lugha za mzazi (kwanza), mielekeo ya wanafunzi kuhusu somo lenyewe, uhaba wa vifaa vya kufundishia (vitabu), ujuzi na tajriba ya mwalimu pamoja na ukosefu wa walimu wa kutosha.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

**Chati 3: Chngamoto za walimu na wanafunzi; Maoni ya walimu**




Kwa mujibu wa walimu, changamoto karibu zote zilitawala Kisumu. Hata hivyo, changamoto za wanafunzi kutoshirikiana na wenzao kujifunza, kutumia mbinu za jadi kufunzia, walimu waliohitimu kuwa wachache na kutowaendea walimu kuelekezwa zilishuhudiwa kiasi Kakamega. Matokeo haya yanaonyesha kuwa wengi wa wanafunzi walipenda kujifunza kivyao huku wakikosa kupata maelekezo ya wenzao au hata ya walimu wao. Wanafunzi hawa huenda walifuatilia mtazamo wa wanaelimu-jamii au wanasosholojia wanaoamini kuwa kazi inapofanywa kibinafsi, mwanafunzi huwajibika zaidi kuliko akiwa katika kundi, hivyo basi, huifanya kazi kwa bidii ili kuiboresha. Hii ni kwa kuwa yeye hufahamu kuwa asipoifanya kazi hiyo vizuri, atakayeumia kwa kupewa alama chache ni yeye mwenyewe (Onyango, 2008).

Matokeo haya yanaonyesha wazi kuwa wazazi wengi wa wanafunzi Kisumu hawakuhusika sana katika ujifunzaji wa watoto wao katika somo la Kiswahili ili kuimarisha ujuzi wao somoni na waliohusika nao hawakuhusika mara kwa mara bali wa Kakamega walionekana kujikaza; waliweza kuhusika kiasi. Hali hii inaweza kuelezwa kuwa ndiyo sababu inayowafanya wanafunzi wengi hasa wa Kisumu kuzembea somoni na hatimaye kutofanya vyema kwalo. Madai haya yanaoana na maoni ya Mwakarayz (2011) anayewataja wazazi kama kikwazo kikuu cha maendeleo ya somo la Kiswahili na vilevile lugha ya Sheng'. Matokeo haya yanalingana na maoni ya Owala (2014) kuwa ni wajibu wa wazazi kuwaelekeza watoto wanaporudi nyumbani kutoka shuleni. Kwa mfano, watoto wanapopewa mazoezi ya ziada, wazazi wanastahili kuwa katika mstari wa mbele kuhakikisha kuwa kazi hiyo imefanywa vyema. Ikiwa wamefanya makosa katika mazungumzo yao, wazazi waweze kuwarekebisha bila kuwaaibisha (kuwatia aibu kwa namna yoyote ile). Yaani wazazi wawe vielelezo kwa ujifunzaji L2 kwa wana wao hasa wakiwa manyumbani mwao.

Idadi ya wanafunzi madarasani ilionekana kuwa tatizo kuu kwa walimu; asilimia 72.7 Kakamega na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

50 Kisumu ilikadiria kuwa wanafunzi walikuwa wengi mno madarasani. Maoni haya yanalingana na madai ya wakuu wa Idara Kakamega waliosema haya;

> *"Idadi kubwa ya wanafunzi yazuia mwalimu kufikia kila mmoja wao hivyo kuathiri umilisi wao wa lugha"* (MK 16- mjini).

> *"Tatizo letu ni kuwa, kuna idadi kubwa ya wanafunzi katika madarasa yetu"* (MK 3-mjini).

> *"Kuna uwingi wa kazi miongoni mwa walimu kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi hali inayoathiri utendakazi wetu"* (MK 20-shambani).

> *"Idadi ya wanafunzi madarasani mwetu iko juu sana" (MK 1-shambani).*

Kulingana na madai haya ni wazi kuwa hata walimu wenyewe walikiri kuwa kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi hawangepata muda wa kutosha wa kumshughulikia kila mwanafunzi kwa ukamilifu hivyo kuathiri kwa njia hasi ujifunzaji wao. Maoni haya yaliwiana na matokeo ya Melly (2019) aligundua kuwa wanafunzi katika shule za upili wamekuwa wengi sana hali inayotatiza sana matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji.

Walimu walibainika kuwa ni wachache mno katika shule mbalimbali hivyo kuwa na changamoto kuu katika ufunzaji wa Kiswahili. Matokeo haya yaliungwa mkono na wakuu wa Idara ya Kiswahili Kisumu na Kakamega mtawalia;

> *"Kazi ni nyingi; muda ni mchache na mwalimu ni mmoja tu shuleni*" (MK 19 KSM shambani).

> *"Walimu ni wachache kutokana na kwa na tume husika TSC kukosa kuwaajiri walimu wa kutosha"* (MK 4 KSM mjini).

> *"Idadi ndogo ya walimu shuleni huwafanya wawe na kazi nyingi"* (MK 23 KK mjini).

> *"Tuna vipindi vingi kutokana na idadi ndogo ya walimu shuleni hali inayoathiri utendakazi wetu kama walimu"* (MK 20 KK shambani).

Maoni haya yanalingana na ya Oloo (2018) aliyedhihirisha kuwa changamoto au mambo yanayoathiri ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili na matokeo yao ni kama vile uhaba wa walimu, uhaba wa vifaa, maandalizi mabaya ya walimu na mielekeo hasi ya walimu na wanafunzi kuhusu vipengee fulani katika somo la Kiswahili.

Pia, walimu walilazimika kufunza vipindi vingi kwa sababu ya uhaba wa walimu wa Kiswahili ambao hufunza masomo mengine pia hasa yanayofunzwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza kama lugha ya kufunzia. Wakuu hawa walitoa kauli zifuatazo kuhusu utendakazi wao;

> *"Walimu hufunza masomo yao ya pili pamoja na Kiswahili hivyo wakati mwingine wanakabiliwa na wakati mgumu wa kuyapangia masomo yote mawili wanayoyafunza"* (MK 22 KK shambani).

> *"Kando na somo la Kiswahili, walimu hulazimika kufunza masomo mengine- lile somo la pili alilolisomea chuni"* (MK4 KSM mjini).

> *"Shuleni mwetu walimu wa kiswahili wanafunza somo la pili na Kiswahili" (MK11 KK mjini).*

Madai haya yanawiana na maoni ya Oloo (2018) kuwa walimu walidai kuwa wanafanya kazi nyingi sana ambazo hazikuwaruhusu kutafuta nyenzoza kufunzia madhali walipewa vipindi vingi vya Kiswahili na masomo mengine kama vile Historia, Jiografia, Hisabati na Dini. Kulingana naye, walimu wana kazi nyingi za kutekeleza ili kukamilisha silabasi ya Kiswahili na kuwa kazi hizo zao nyingi ni kigezo kikuu zaidi kinachowazuia kuteua na kutumia mbinu mwafaka katika ufunzaji na ujifunzaji wao.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

Isitoshe, walimu hawa waliishia kutawala shughuli za ufunzaji na ujifunzaji wa somo hili madarasani mwao. Asilimia 33.3 ya walimu Kakamega na 50 Kisumu walikubali kuwa walitawala masomo ya Kiswahili madarasani mwao. Hii inaashiria kuwa walimu walikuwa na mwelekeo hasi kuhusu ushirikishi wa wanafunzi kikamilifu masomoni; wachache tu ndio waliotumia mbinu ya ugunduzi inayowapa fursa wanafunzi kuyatawala masomo yao na kujigundulia mambo kivyao. Mbinu ya ugunduzi ndiyo inayopendekezwa na watafiti wengi wa L2 kwani kiasi kidogo sana cha sintaksia ya lugha ndicho mtu anaweza kufunzwa madhali mambo mengi sana mtu mwenyew hujigundulia. Matokeo haya yanaoana na maoni ya Chika (2012) kuwa kujifunza hufaulu zaidi wanafunzi wanapohusishwa katika mambo yote yanayotendeka madarasani kwa kuuliza maswali na kutawala maongezi. Hata hivyo, walimu katika kaunti ya Kisumu walitawala sana ufunzaji na ujifunzaji hali iliyochangia katika wanafunzi wao kutofuzu vyema katika somo la Kiswahili (Rejelea kielelezo cha matokeo).

Mwelekeo mseto ulikosa kuzingatiwa pakubwa katika ufunzaji wa Kiswahili na walimu wengi licha ya kuwa ndio mtindo unaopendekezwa utumiwe kufunzia Lugha na Fasihi ya Kiswahili na kutambua manufaa yake. Asilimia 33.3 na 33.3 yao katika kaunti za Kakamega na Kisumu mtawalia walikubali kuwa walitumia mbinu mseto kufunzia somo la Kiswahili madarasani mwao. Vilevile, ulikadiriwa kuwa na manufaa makuu kwa asilimia 75 (n=9) na 83.3 (n=10), manufaa ya wastani kwa asilimia 18.2 (n=2) na 8.3 (n=1) Kakamega na Kisumu kimfuatano. Inawezekana kuwa hali hii ilichangiwa sana na ujuzi walio nao walimu katika usetaji wa mada za somo la Kiswahili. Madai haya yanawiana na maoni ya Odhiambo (2012) aliyegundua kuwa mtaala kupitia utaratibu wa kusetwa kwa masomo ulikuwa mpana zaidi na kuwa walimu hawajapata maandalizi ya kutosha kulingana na matumizi ya mbinu mseto. Matokeo ya wanafunzi yaliweza kuathirika sana katika som madhali mbinu hii haikutumiwa ipasavyo kufunzia. Madai haya yanalingana na ya Wanyama (2007) aliyesisitiza kuwa matumizi ya mwelekeo mseto katika Kiswahili, wepesi wa kueleweka kwa uwasilishaji wa mwalimu na matumizi ya mbinu bora za kufundishia yanahusiana moja kwa moja na matokeo ya wanafunzi katika mtihani.

Ni wazi kuwa mbinu hii ina manufaa makuu katika elimu ndiposa silabasi ya K.I.E 2002 ilipendekeza ufundishaji wa lugha kwa kuzingatia mwelekeo mseto ambao unawapa wanafunzi ushiriki mkubwa wakati wa ufunzaji na ujifunzaji wao (Opunde, Haijulikani). Hata hivyo, walimu wa Kisumu walionekana kuthamini sana hali ya kutenganisha Lugha na Fasihi ya Kiswahili. Hii ni kwa kuwa asilimia 83.3 (n=10) yao ilidhihirisha manufaa makuu ya kuzitenganisha Kisumu huku asilimia 75 (n=9) ikiunga mkono maoni haya Kakamega. Hii ilidhihirisha wazi kuwa walimu walitamani Lugha na Fasihi zitenganishwa kama masomo mawili tofauti. Matokeo haya yanawiana na mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Koech (1999) kuwa masomo ya Lugha ya Kiswahili na Fasihi ya Kiswahili yafundishwe kama masomo mawili tofauti. Maoni haya yalilingana na ya Rutere (2012) kuwa walimu wengi walikuwa na mwelekeo hasi kuhusu usetaji wa mada za Kiswahili; Lugha na Fasihi; kwao mada hizo zilistahili kufunzwa kama masomo mawili tofauti.

Walimu walijiamini katika ufunzaji wao wa somo la Kiswahili bali wengine hawakujiamini hivyo kuathiri ufunzaji wao. Walimu wengi waliokuwa na tajriba kuu katika ufunzaji walipatikana Kakamega hali inayoweza kueleza kwa nini walimu walijiamini zaidi Kakamega wakilinganishwa na wenzao wa Kisumu. Hali hii inadhihirisha kwa nini wanafunzi wa Kakamega waliweza kufanya vyema zaidi katika mtihani wa insha ya kiubunifu walipolinganishwa na wenzao wa Kisumu. Walimu walitambulisha kuwa wakiwa na tajriba kuu katika ufunzaji wao hupata kujiamini zaidi na kuwawezesha kuwaelewa wanafunzi wao vyema zaidi hasa kufahamu mahitaji ya kila mmoja wao na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

kuwashughulikia vilivyo. Isitoshe, waliweza kuelewa mada zote walizozifunza vizuri sana huku wakipata kujiamini katika ufunzaji na utendakazi wao kwa jumla (Rutere, 2012).

Mielekeo hasi ya wanafunzi kuhusu somo pamoja na uhaba wa vifaa vya kufunzia na kujifunzia ilikuwa changamoto miongoni mwa walimu hivyo kuathiri ufunzaji na ujifunzaji. Athari ya mielekeo hubainika wazi katika ujifunzaji na utendaji wa wanafunzi wenyewe madhali wakiwa na mwelekeo chanya kuhusu lugha wanayojifunza wao hupata kufanikiwa na hujifunza haraka kuliko wenzao wenye mwelekeo hasi (Onyango, 2008). Kulingana na wakuu wawili wa Idara Kisumu (mjini);

> *"Uhaba wa vitabu ni tatizo kuu kwani baadhi ya wanafunzi hukosa kununua vitabu viteule (set books) jambo linalotatiza sana ufunzaji wa Fasihi Andishi"* MK 18.

> *"Mara nyingine hamna nyenzo ya kusaidia katika utekelezaji wa shughuli ya kufunza" MK 2.*

Matokeo haya ni sawa na ya Wambua na wengine (2019) waliosema kuwa uhaba na ukosefu wa vifaa vya kufunzia umebainika kuwa changamoto kuu katika utekelezaji wa mtaala kikamilifu nchini Kenya. Pia, yalilingana na ya Mbito (2013) aliyetaja uhaba wa vitabu kama changamoto kuu iliyowakumba walimu na wanafunzi katika shughuli nzima ya ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili hasa zile za umma. Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa vifaa vingine vilikuwa na vikwazo vya hapa na pale katika ufunzaji. Ilikuwa wazi kuwa walimu walikabiliana na changamoto za makosa na mambo yaliyopotosha au hata kukanganya yaliyopatikana katika baadhi ya vitabu vilivyotumiwa katika ujifunzaji. Mkuu mmoja wa idara Kakamega (mjini) aliweza kudhihirisha kuwa kuna changamoto katika kitengo cha uandishi wa vitabu vinavyotumika katika ufunzaji;

> *"Baadhi ya waandishi wameshughulikia vipengele fulani kwa kiwango cha kutiliwa shaka au kwa njia ya kukanganya kwa mfano baadhi ya mambo katika Uhondo wa Kiswahili hasa kitabu cha wanafunzi wa kidato cha kwanza. Istilahi hazifafanuliwi vyema, mwalimu analazimika kujitafutia njia mbadala za kujijazia haya"* (MK 11).

Aidha, kuna wakuu wa idara wengine hasa wa mijini waliotambua baadhi ya changamoto walizozigundua kama zifuatazo;

> *"Makosa ya kisarufi ni mengi huku mada ya viambishi ikizingatiwa kijuujuu kwani hata aina zake hazikubainishwa. Kwenye vitamkwa- sauti ya mdomoni /m/ haipo, maelezo ya ngeli za nomino ni finyu mno na mifano michache sana hutolewa"* (MK 3 KK).

> *"Kitabu cha Uhondo kina shida zake tu. Pia, masuala ya Isimujamii hayajashughulikiwa kamwe, mada za insha haziangaziwi kwa kina, maelezo ni mafupi na hakuna mifano na maelekezi mwafaka hasa uandishi wa hotuba"* (MK 16 KK).

Maoni haya pia yalilingana na kauli za baadhi ya walimu hasa wale waliofunza mijini;

> *"Makosa ya uchapishaji yanajitokeza kwa wingi katika Uhondo wa Kiswahili huku mada zake pia zikijadiliwa kijuujuu hivyo kuzifanya ziwe finyu"* (Mwl 1 KSM)

> *"Maendelezo ya maneno yana kasoro (makosa ya sarufi na hijai yametawala) na mada zake zimeshughulikiwa kwa namna finyu"* (Mwl 17 KSM).

Maoni haya yalilingana na ya Akaka (Haijulikani) kuwa waandishi wa vitabu hutofautiana katika masuala tofauti kuhusu vipengele vya lugha kwa sababu ya mielekeo yao inayotofautiana kinadharia. Tofauti hizi humwacha mwalimu wa lugha ya Kiswahili ambaye haelewi vyema nadharia hizo za

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

sarufi katika njia panda. Hata ingawa Taasisi ya Elimu nchini imetoa orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa inakuwa nje ya uwezo wa mwalimu kuwazuia wanafunzi kusoma vile ambavyo havijapendekezwa. Waandishi wengi bandia wamechipuka na kuchapisha vitabu vinavyosambazwa katika soko huria la vitabu kwa bei nafuu ikilinganishwa na bei ya vitabu vilivyoidhinishwa. Ni changamoto kuu kwa mwalimu anayefunza Kiswahili kurekebisha mambo ambayo wanafunzi hawa washajifunza kutoka kwenye vitabu hivyo bandia. Zaidi ya hayo, wachapishaji nao huchangia sana katika kuchapisha vitabu vya viwango vya chini; wanakosa kuvitathmini vitabu hivyo kimakini kwa sababu zao ambazo ni za kibinafsi.

Hata hivyo, baadhi ya vipengele vimeangaziwa kikamilifu kama ufahamu kushughulikia masuala ibuka na maswali yake kufaa zaidi- yanalingana na viwango vya wanafunzi na mada (taarifa) huwiana na tajriba zao. Maoni haya yalioana na kauli iliyotolewa na mwalimu mmoja aliyefunza katika shule ya mjini kaunti ya Kakamega;

> *"Ingawaje kitabu cha Uhondo wa Kiswahili cha wanafunzi wa kidato cha kwanza kina mapungufu mengi, kina mambo mazuri kwani mada zinazolingana na maswala ibuka katika jamii yetu huzingatwa katika fahamu zake na maswali yake ya udurusu pia ni mazuri"* (Mwl 22).

> *"Kuna makosa chungu nzima katika Uhondo lakini kina mafunzo mazuri kupitia taarifa zake kwani Ufahamu hugusia sana masuala ibuka na maswali yake pia ni mazuri; yametungwa vilivyo kulingana na ujumbe wa taarifa hizo"* (MK 23 KK ).

Maoni haya yanalingana na maoni ya Akaka (Haijulikani) aliyedokeza kuwa waandishi wa vitabu hutofautiana katika masuala tofauti kuhusu vipengele vya lugha kwa sababu ya mielekeo yao inayotofautiana kinadharia. Tofauti hizi humwacha mwalimu wa lugha ya Kiswahili asiye na uelewa wa nadharia hizo za sarufi katika njia panda. Pia, wachapishaji nao huchangia sana katika kuchapisha vitabu vya viwango vya chini; wankosa kuvitathmini vitabu hivyo kimakini kwa sababu zao binafsi. Maoni haya yanawiana na ya Rutere (2012) kuwa mitindo tofauti inatumiwa na wachapishaji wa vitabu hivyo kuwakanganya walimu pamoja na wanafunzi.

Ufunzaji wa Kiswahili kwa kutumia vifaa vya kidijitali unalingana na mapendekezo ya Koross na Murunga (2017) kuwa, katika karne ya ishirini na moja, ufunzaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili lazima uchukue mkondo wa kuhusisha matumizi ya teknolojia ya kisasa. Aidha, unasawiana na maoni ya Melly (2019) aliyesisistiza kuwa mwalimu katika shule ya kisasa hana budi kuhusisha vifaa vya kisasa; kidijitali ili kuweza kuteka ari ya wanafunzi ya kutaka kujifunza zaidi na hatimaye kuimarisha umilisi wao na matokeo yao katika somo la Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanabainisha kuwa vifaa vya kitambo vilionekana kutawala katika ufunzaji wa Kiswahili katika madarasa ya Kakamega kuliko hali ilivyokadiriwa kuwa Kisumu. Hivyo, ni wazi kuwa matumizi ya vifaa vya kisasa (kidijitali) hayakutiliwa maanani; si kamilifu hivyo walimu na wanafunzi hawapati matokeo bora ya ufunzaji na ujifunzaji wao. Matokeo haya yalilingana na maoni ya Miima (2014) kuwa walimu wachache tu ndio waliotumia vifaa vya kidijitali kufunzia lugha ya Kiswahili, wengi wao walifurahia na kuridhika kutumia mbinu za kijadi au za kawaida kufunzia.

Matokeo ya utafiti huu kupitia mitazamo na mahojiano yalionyesha kuwa shule katika kaunti ya Kakamega zilikuwa na maktaba kuliko hali ilivyokuwa Kisumu. Maktaba zilipatikana katika shule nyingi kwa asilimia 66.7 (n=8) Kakamega huku asilimia 25 (n=3) ikiwa nazo Kisumu na asilimia 8.3 (n=1) ikihifadhi vitabu vya Kiswahili idarani Kisumu, asilimia 33.3 (n=4) na 58.3 (n=7) zikiwa na ghala au stoo ya kuhifadhia vitabu Kakamega na Kisumu mtawalia huku asilimia 8.3

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

(n=1) ikikosa hata stoo ya vitabu Kisumu. Ukosefu wa maktaba uliwanyima wanafunzi katika kaunti ya Kisumu nafasi mwafaka ya kuimarisha ujuzi wao wa lugha; jambo linaloweza kuwa ndilo ni mojawapo za sababu ya matokeo duni katika somo la Kiswahili humo. Matokeo haya yanalingana na ya Njoroge na Ndiragu (2018) waliobainisha kuwa ukosefu wa vifaa maalum kama maktaba na vifaa vya kufunza na kujifunza ulikuwa na athari hasi kwa matokeo ya wanafunzi bali uwepo wa vifaa hivyo uliathiri matokeo yao kwa njia chanya. Madai haya yanaoana na ya Mutsotso na Nasongo (2013) waliogundua kuwa ukosefu wa vifaa vya kufunzia na maktaba ulikuwa na athari hasi kwa matokeo ya wanafunzi. Matokeo haya huingiliana na ya Ogero (2012) aliyegundua kuwa kukosekana kwa maktaba kuliwanyima wanafunzi muda mwafaka wa kujifunza kwa kuchambua, kusoma kwa kina zaidi na kuingiliana kikamilifu na mada za somo kwenye vitabu mbalimbali hivyo kuathiri ujuzi wao wa lugha na hatimaye matokeo yao.

**Visababishi vya Changamoto**

Kwanza kabisa, uhaba wa walimu ulizingatiwa kama kikwazo katika maandalizi na utendakazi wenyewe. Mkuu mmoja wa idara kaunti ya Kisumu (mashambani) alisema; "*kazi ni nyingi, muda ni mchache na mwalimu ni mmoja tu*" (MK 19). Mkuu wa idara Kakamega (shambani) aliunga mkono maoni haya; "*serikali kukosa kuajiri walimu husababisha changamoto katika utendakazi wetu kama walimu wa Kiswahili*" (MK 15). Mwingine wa Kisumu (mjini) alisisitiza; "*kwa kutoajiri walimu wa kutosha na tume husika TSC, walimu ni wachache bali wanalazimika kufunza somo lingine*" (MK 4).

Pili, walimu wa Kiswahili walilazimika kufunza masomo yao ya pili katika shule nyingi (karibu shule zote) hivyo kusababisha walimu hao kuwa na kazi nyingi mno hivyo kuwa na ugumu wa kujiandaa kikamilifu katika masomo haya mawili. Mudir mmoja wa Kakamega (mashambani) alisema; "*Wakati mwingine walimu wanakabiliwa na wakati mgumu kuyapangia masomo yote mawili wanayoyafunza*" (MK 22). Mmoja wa Kisumu (mjini) akasema; "*Walimu wengine wa Kiswahili wana kazi nyingi mno*" (MK 17). Maoni haya yanalingana na madai ya Kolawole (2002), Nwanekezi (2006) na Gekombe (2015) waliobainisha kuwa idadi ya vipindi alivyokuwa navyo mwalimu iliathiri sana matokeo ya wanafunzi wao somoni. Kulingana nao, kulionekana kuwa kuna uhusiano wa karibu sana kuhusu kazi alizokuwa nazo mwalimu na matokeo ya wanafunzi wao; kuwa idadi kubwa ya vipindi ilisababisha matokeo duni huku idadi ndogo ikisababisha matokeo mema. Isitoshe, maoni haya yanaoana na maoni ya Oloo (2018) kuwa walimu walidai kuwa wanafanya kazi nyingi sana zisizowaruhusu kujiandaa kwa kutafuta nyenzo na kutumia mbinu bora za ufundishaji kwa kuwa walipewa vipindi vingi vya Kiswahili na masomo mengine.

Kando na hayo, idadi ya wanafunzi ilisababisha kuwepo kwa changamoto katika utendakazi kwani wakiwa wengi si rahisi kuwapa mazoezi ya kutosha kila mara na kuyasahihisha kwa ukamilifu. Mkuu mmoja kaunti ya Kakamega (mashambani) alidhihirisha haya; "*Idadi ya wanafunzi darasani ni juu hivyo kutatiza shughuli ya kuwatathmini vyema*" (MK 1). Matokeo haya yanawiana na maoni ya Owala (2014) kuwa ikiwa wanafunzi wamefurika katika madarasa yao, mwalimu hana uwezo wa kuwashughulikia wanafunzi wake kibinafsi.

Muda uliotengewa somo ulikadiriwa kuwa haukutosha kulingana na mada zake hivyo kutatiza utendakazi wa walimu.Maoni haya yalizingatiwa na mkuu wa idara mmoja katika kaunti ya Kisumu (mashambani) aliyesema kuwa; "*Wakati mwingine muda huwa mchache kwa mada iliyoteuliwa ndiposa mwalimu hukosa kuwapa mazoezi*" (MK 5). Matokeo haya ni sawa na ya Oloo (2018) aliyegundua kuwa kulikuwa na uzembe miongoni mwa walimu wa kutafuta nyenzo,ukosefu wa muda wa kujitayarisha na kutafuta nyenzo kwani muda wenyewe ulikuwa ni mfupi; hautoshi. Aidha, maoni haya yanawiana na ya Chacha (2016) kuwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Kiswahili hakijapewa muda wa kutosha kwani vipindi vilivyotengewa somo kwa wiki ni vichache.

Pia, aina na eneo la shule lilitajwa kama sababu ya kuwepo kwa changamoto kama vile ukosefu wa vifaa mbalimbali vya kufundishia kama vile vifaa vya kidijitali, vitabu viteule vya fasihi andishi, vitabu vya ziada pamoja na vya kudurusu na kufanyia mazoezi. Kulingana na mkuu mmoja Kakamega (mashambani), "*Eneo la shule lina athari kuu iliyo hasi; vifaa vya kufunzia hukosekana katika shule za mashambani hasa vifaa vya kidijitali, vitabu vya kudurusu, vya kiada kiasi, vya ziada pamoja na vile vya fasihi (vitabu viteule), hivyo shughuli nzima ya ufunzaji na ujifunzaji hutatizwa*" (MK 15). Uhaba na ukosefu wa vifaa hivyo viliwaacha walimu hawa katika njia panda; wajitafutie au wavipuuze katika ufunzaji wao. Kama inavyobainika, wengi walivipuuza na kutumia mitindo ya jadi ya kufunzia hivyo kuathiri ujifunzaji na matokeo yawanafunzi wao. Maoni haya yanawiana na ya Melly (2019) aliyebainisha kuwa walimu bado waliendelea kutumia sana mbinu za jadi kufundishia Kiswahili.Aidha, yalilingana na maoni ya Wambua na wengine (2019) aliyeshikilia kuwa vifaa vya kufunzia na kujifunzia huathiri kwa namna chanya matokeo ya wanafunzi katika somo hivyo ukosefu wao huweza kusababisha matokeo kuwa mabaya au duni.

Mwisho, walimu wengine nao walikosa kujitolea kikamilifu katika kutekeleza majukumu yao ya kuwafunza na kuwaelekeza wanafunzi ndiposa walipata ugumu wa kuandaa vifaa maalum pamoja na nakala za kufunzia. Chambilecho wakuu wawili wa idara kaunti ya Kisumu (mjini); "*Walimu wana tabia ya kutojitolea kazini*" (MK 14) huku mwingine akisisistiza haya; "*Walimu wamekosa kujitolea kikamilifu kazini*" (MK 24). Maoni haya pia yalibainishwa na mwanafunzi mmoja wa Kisumu mashambani; *"Mwalimu hukosa kuja darasani na hata shuleni mara kadhaa hivyo hatupati kusoma na kujifunza Kiswahili kama inavyofaa"* (Mwanafunzi 328). Isitoshe, matokeo ya utafiti huu yanalingana na maoni ya Ruddell (2002) kuwa ingawa walimu wengi wa lugha wamefuzu vyema na kuwa na uwezo wa kufundisha inavyostahili, wengi hawajizatiti kuweka mikakati bora ya kufundishia jambo linalosababisha matokeo ya Kiswahili kuwa duni. Hali hii hutokea licha ya wao kufahamu kuwa mbinu wanazozotumia kufunzia si bora na kuwa hawajukumiki katika majukumu hayo kama inavyostahili. Maoni haya yanawiana na Owala (2014) aliyegundua kuwa walimu wengi aliowatifiti walieleza kwamba wanakosa motisha katika kufunza. Pia, wanafunzi walielezea kuwa waimu wao walikosa kuhudhuria masomo yao ya Kiswahili hivyo kuathiri ujifunzaji wao na kuwafanya wawe na mielekeo hasi kwa somo lenyewe.

## Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto Mbalimbali

### *Mikakati ya Wanafunzi*


Mbinu zilizotumiwa zaidi Kakamega zilikuwa kushirikiana na wenzao na kuwaendea walimu ili waelekezwe huku Kisumu zilikuwa kupambana kivyao na kuwaendea walimu kuelekezwa. Wanafunzi wa Kakamega waliwashirikisha walimu wao zaidi katika ujifunzaji wao kuliko wa Kisumu waliojitetea wenyewe kwa kujitegemea kuwashinda wenzao wa Kakamega. Hali hii inadhihirisha kuwa iwapo wanafunzi hawa wa Kisumu walishindwa kukabiliana na hali fulani katika somo waliishia kutolifahamu hivyo kutoboresha ujuzi wao katika somo huku wale wa Kakamega wakipata maelekezi yanayofaa pamoja na kuazima vitabu vinavyowafaa hivyo kupata fursa nzuri ya kuimarisha ujuzi wao katika lugha hata zaidi. Isitoshe, wanafunzi hao walivitumia vifaa hivyo kutoka kwa walimu wao kuimarisha ujuzi wao katika somo pamoja na wenzao ambao nao walikuwa wamevikosa. Mtazamo huu unalingana na wa Wambua na wengine (2019) aliyeripoti kuwa walimu na wanafunzi huazima vifaa vya kufunza na kujifunza Kiswahili kutoka shule jirani au hata jamaa zao waliokuwa navyo ambao nao waliweza kuvitumia

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

pamoja na wenzao waliovikosa kisha wakavirudisha kwa wenyewe baada ya kuvitumia.

**Chati 4: Mikakati ya wanafunzi**




Wanafunzi wa Kakamega walionekana kufurahia mbinu ya kushirikiana na wenzao kuliko wenzao wa Kisumu, walionekana kuelewa fika umuhimu wa kujadiliana na wenzao katika kukuza na kuimarisha ujuzi wao wa lugha. Miingilano hii iliwawezesha kufuzu zaidi katika somo wakilinganishwa na wenzao waliokosa kuthamini mbinu hii kikamilifu (Rejelea kielelezo kifuatacho cha matokeo). Maoni haya yanalingana na yale ya Owala (2014) aliyebainisha kuwa wanafunzi wanaofanya kazi katika makundi huwa na matokeo mazuri katika mitihani yao na vilevile sifa ya juu ya kujistahi.

**Jedwali 1: Matokeo ya Wanafunzi katika Insha ya Ubunifu**

| Vigeu | Viwango | Mean/Wastani | (Standard Deviation) kupotoka kwa kawaida | Alama ya chini | Alama ya juu |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaunti | Kakamega | 49.12 | 16.14 | 16 | 88 |
| | Kisumu | 44.00 | 12.82 | 4 | 84 |
| Eneo la shule | Mashambani | 42.66 | 13.97 | 4 | 80 |
| | Mijini | 50.83 | 14.98 | 12 | 88 |
| Jinsia | Wavulana | 48.27 | 13.88 | 12 | 88 |
| | Wasichana | 45.94 | 15.95 | 4 | 88 |
| Mielekeo | Hasi | 42.26 | 13.90 | 16 | 68 |
| | Chanya | 47.92 | 14.92 | 4 | 88 |
| | Sina uhakika | 43.28 | 15.13 | 12 | 80 |
| | Sijui | 35.56 | 16.68 | 16 | 76 |
| Ufaafu na utoshelevu wa mazoezi | Unafaa zaidi | 47.35 | 14.84 | 4 | 88 |
| | Unafaa kiasi | 45.95 | 15.59 | 12 | 88 |
| | Haufai kamwe | 43.41 | 16.89 | 16 | 76 |
| Kategoria ya shule | Wavulana | 47.60 | 16.41 | 4 | 88 |
| | Wasichana | 50.02 | 14.10 | 20 | 88 |
| | Mseto | 44.45 | 13.90 | 12 | 84 |
| Jinsia za shule mseto | Wavulana | 42-67 | 14.37 | 12 | 80 |
| | Wasichana | 46.05 | 13.30 | 12 | 84 |

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

Mikakati zaidi iliyobainishwa kuwa ilizingatiwa ilikuwa;

- Kudurusu vitabu na kutafiti zaidi kuhusu mada za Kiswahili kutoka kwenye majarida na vitabu vya marejeleo katika maktaba ya kitaifa/ya umma.
- Kujitafutia vibarua ili wapate pesa za kununua vifurushi vya data "bundles" na za muda wa maongezi "airtime" ili wadurusu na kutafiti zaidi mtandaoni.
- Kujitengea mahali pasipo na kelele ili wajisomee na kudurusu mada mbalimbali katika somo.
- Kujitengea muda wa kujisomea na kudurusu mada za Kiswahili wasizozielewa vyema.

Wanafunzi hawa walidurusu mada za somo hili ili kuimarisha ujuzi wao kwalo. Hata hivyo, wanafunzi wa Kakamega walionekana kudurusu sana somo la Kiswahili wakilinganishwa na wenzao wa Kisumu hali ambayo iliwawezesha kuimudu lugha kwa ufasaha zaidi kuwashinda wenzao. Hali hii iliwawezesha kusoma machapisho mengi ya L2 na kujiongezea maarifa kwayo huku wakilenga kupata alama za juu katika mitihani ya lugha husika.

Vilevile, usomaji wa vitabu vya hadithi vya Kiswahili ilizingatiwa japo usomaji huo ulionekana kuendelezwa zaidi kila mara Kakamega kuliko hali ilivyokuwa Kisumu. Wanafunzi hujifunza mambo mengi kutokana na usomaji huo; ubunifu, sarufi na misamiati ya lugha husika na kutambua jinsi maneno fulani huendelezwa pamoja na kutumika kwao kimuktadha. Ni kutokana na mkakati huu uliozingatiwa na wanafunzi katika ujifunzaji wao wa somo ndiko wanafunzi wa Kakamega waliweza kuonyesha viwango vya juu vya umilisi wa lugha hii kushinda wenzao wa Kisumu kijumla na hasa katika insha ya kiubunifu waliyoiandika. Madai haya yanawiana na ya Chacha (2016), aliyesisitiza kuwa usomaji wa vitabu vya hadithi una manufaa katika ukuzaji wa umilisi wa lugha ya Kiswahili katika viwango mbalimbali vya masomo nchini Kenya. Usomaji huu huwa na uhusiano na stadi zote za kujifunza lugha ya Kiswahili (kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika). Mwanafunzi asipoimudu lugha hawezi kufanya vizuri katika mtihani wa somo la Kiswahili.

**Maoni ya Walimu Kuhusu Mikakati Ya Wanafunzi Wao**

Wakuu wa idara waliweza kutaja baadhi ya mikakati iliyotumiwa na wanafunzi wao pamoja nao kama walimu katika kupambana na changamoto walizopatana nazo. Mwanzo, wanafunzi walijitafutia muda zaidi ya kujifunza na kudurusu mada mbalimbali katika somo la Kiswahili wakati wa asubuhi na jioni kabla na baada ya masomo yao ya kawaida. Chambilecho mkuu mmoja Kakamega (mjini); "*Wao hutenga muda wa ziada asubuhi na jioni baada ya madarasa na vipindi vya kila siku ili waweze kudurusu"* (MK13). Maoni haya yanalingana na ya Simiyu (2013) aliyebainisha kuwa kukamilisha silabasi kwa wakati ufaao huathiri kwa njia chanya matokeo ya wanafunzi kwani wanafunzi hupata kujiamini na kuondoa hofu inayochangia na kuathiri kwa njia hasi matokeo yao. Walimu na wanafunzi katika shule zinazofanya vyema katika mitihani ya kitaifa hujitafutia muda mbadala wa kuwawezesha kukamilisha silabasi mapema na kukuza uelewaji wa mada hizo miongoni mwa wanafunzi wao.

Pili, walihakikisha kuwa wanajadiliana na wenzao katika makundi huku wakifanya mazoezi ya ziada na kuelekezana kuhusu masuala ya Kiswahili. Mkuu mmoja Kakamega (mjini) alidhihirisha kuwa; "*Wanafanya kazi katika makundi, kazi mradi na mazoezi ya lazima waliypopewa kwa pamoja wakielimishana vilivyo"* (MK 11). Madai haya yalikuwa sawa na ya Kanga'hi (2012) na Roblyer (2006) waliobainisha kuwa wanafunzi walijifunza vyema na kwa urahisi katika makundi kwa kuwa waliweza kuelewa na kukumbuka walichojadiliano kukihusu. Kulingana nao, maarifa huibuliwa na kukuzwa kupitia maingiliano na tajriba za

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

wanafunzi kuliko ufunzaji unaotawaliwa na walimu wao.

Tatu, wanafunzi huamua kufanya mazoezi na kazi mradi kivyao bila kusubiri wapewe na walimu wao kisha wao hujitahidi kuwapelekea walimu wazipitie na kuwakosoa au hata kuwaelekeza panapofaa. Mkuu wa idara mmoja Kisumu (mjini) alidhihirisha kuwa; "*Wanafunzi wana makundi wanayoyatumia kushauriana baina yao wenyewe, wakishindwa hutafuta uelekezi kutoka kwa walimu"* (MK 21). Mkuu mwingine wa idara Kakamega (mashambani) akasisitiza haya; "*Wao hujituma kikamilifu kwa kuwaendea walimu wawaelekeze*" (MK 22). Maono haya yanaoana na ya Oloo (2018) aliyebainisha kuwa wanafunzi wenye mielekeo chanya kuhusu somo hilo, hutumia muda wao mwingi sana kufanya mazoezi katika somo hilo.

Nne, kuna walioamua kupambana na hali zao binafsi; hawakutafuta maelekezi kutoka kwa walimu, wenzao, au hata wazazi na walezi wao. Kulingana na mkuu mmoja Kisumu (mashambani); "*Wanaweza kuamua kupambana na hali zao wenyewe*" (MK 19). Tano, wanafunzi wengine walijihusisha na usomaji wa kina ili waweze kukuza ujuzi wao katika somo lenyewe. Kwa mujibu wa mkuu mmoja Kakamega (mashambani); wanafunzi walijikaza kusoma kwa kina na kushauriana kwa kuwauliza walimu mambo na maswali yanayowatatiza katika somo. Mkuu wa idara mwingine Kakamega (mjini) alidhihirisha kuwa; "*Wanajipa motisha kwa kuhimizana na kushauriana kuhusu umuhimu wa kusoma kwa kina na kuwapa ushauri wenzao kufurahia usomaji bila kushinikizwa na walimu*" (MK13).

Sita, waliweza kuhimizana katika ujifunzaji wao na kuwashauri wenzao kupata maelekezo kutoka kwa walimu wao kuhusu somo kila linapobidi na kuwa inafaa huku wakishirikiana vilivyo na walimu wao. Mkuu mmoja wa idara Kisumu (mjini); "*Wanaweza kuhimizana kufanya kazi za ziada na kushauriana na walimu husika*" (MK 17). Maoni haya yalisisistizwa na mkuu mmoja Kakamega (mashambani); "*Wanafunzi werevu wanajaribu jinsi wawezavyo kubadilisha mielekeo yao kwa kupitia ushauri wa walimu wao*" (MK 3).

Mwisho, waliwateua wanafunzi waliofanya vyema katika somo ili wapate kuwafunza, kuwaelekeza na kuwasaidia kudurusu kila anapochelewa mwalimu kufika au hata kukosa kuingia darasani. Chambilecho mkuu mmoja Kisumu (mjini); "*Kila darasa lina kiongozi wa kiswahili anayewaongoza wenzake wakati wa kufanya marudio au mwalimu asipokuwa darasani"* (MK 4). Maoni haya yanalingana na mtazamo wa Mlay (2010) kuwa ufunzaji wa marika hutokea pale ambapo mwanafunzi aliyetatizika katika jambo au mada fulani za somo hutafuta usaidizi ama husaidiwa na mwenzake aliye na uelewa wa juu katika jambo au mada hizo ili apate kuzielewa.

***Mikakati ya Walimu***

Kwanza kabisa, ilibainika kuwa walimu waliweza kuwatumia wanafunzi wenye uwezo mkubwa katika somo kuwafunza na kuwaelekeza wenzao hasa katika makundi madogo madogo au hata darasani (ufunzaji wa marika). Ilitambuliwa kuwa wanafunzi walichangamkia somo zaidi na kujifunza vyema mno wakifunzwa na mmoja wao. Kwa mujibu wa mkuu wa idara Kakamega (mjini);

> *"Matumizi ya ufunzaji rika husaidia sana kwani wao hujifunza vyema zaidi na kwa urahisi huku waliojifunza husalia akilini kwa muda mrefu zaidi"* (MK 9).

Maoni haya yalisistizwa na mkuu mwingine Kakamega (mjini); "*Kutumia baadhi ya wanafunzi kufunza wengine baadhi ya vipengele vya lugha*" (MK 11). Matokeo haya yanalingana na maoni ya Kavoi (2019) kuwa mbinu ya ushirikianao (hasa kutegemea uwezo sawa wa wanafunzi) huimarisha uhusiano wao kupitia kwa kubadilishana mawazo, kusaidiana, kujibu maswali na kutiana motisha. Kila mwanafunzi ana wajibu wa kuchangia kwa ufanisi wanapopewa nafasi sawa ili kufikia lengo la kikundi kwa kumpa sehemu ya swali kujibu. vyama vya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

Kiswahili viliundwa shuleni ili kuwahimiza wanafunzi kulienzi somo na kuwapa nafasi nzuri ya kujiendeleza katika umilisi wake. Chambilecho wakuu wawili wa idara Kisumu (mijini);

> *"Tuliweza kuanzisha chama cha Kiswahili na kuwahimiza wapende somo la kiswahili na kulichukua kama masomo mengine"* (MK 14 na MK 24).

Vilevile, sera za lugha shuleni zilikuzwa na walimu walihakikisha kuwa lugha sanifu imetumiwa kikamilifu kila mara na hasa siku zilizotengewa somo kama Ijumaa na kushiriki katika mijadala mara moja kwa wiki hasa wikendi. Mkuu mmoja wa idara Kisumu (mjini) alieleza; "*Tumeweza kutenga siku ya Kiswahili shuleni na kuhakikisha wanatumia lugha sanifu kila mara pamoja na kuwepo na mijadala kila mara*" (MK 24). Kulingana na mkuu wa idara Kakamega (mjini); "*Tunajitahidi kutumia mijadala zaidi ili kuwapa fursa ya kujieleza na kujihusisha na masuala ya lugha"* MK (11). Matokeo haya yanaonyesha kuwa wanafunzi huhitaji mazingira mwafaka wa kutumia lugha hii na kuweza kuifanyia mazoezi ya kutosha ili wakuze stadi zake kikamilifu. Maoni haya yanalingana na maoni ya Babusa (2010) aliyegundua kuwa tatizo kuu lililoathiri umilisi wa lugha ya Kiswahili ni kukosa mazingira mwafaka ya kufanyia mazoezi lugha iliyofunzwa hivyo kuathiri ujifunzaji wake na hatimaye matokeo ya wanafunzi kwayo.

Pia, walimu waliwashauri wanafunzi kuhusu umuhimu wa somo, namna ya kuweza kulidurusu kwa ufasaha, jinsi ya kusoma na kujibu maswali katika mtihani wa Kiswahili ili waweze kufuzu kwao. Mudir wa Kisumu na Kakamega walisema haya; "*Walimu wanajitahidi kuhimiza wanafunzi kushiriki katika makundi ili wajadiliane, mashauri ili walipende somo na kuwahimiza kuuliza maswali wanaposhindwa kulijibu*" (MK 19); "*Walimu huwaelekeza katika kusoma na kujibu maswali"* (MK 8) na "*Tunawapa ushauri na mawaidha kuhusu umuhimu wa kujifunza na kupita Kiswahili*" (MK 13).

Walimu waliweza kuwatuza wanafunzi wanaofuzu katika somo pamoja na wanaotia bidii masomoni ili kuwahimiza zaidi na kuwapa motisha wenzao nao wajitahidi somoni. Mkuu wa idara Kisumu (mjini) alisema; "*Kama walimu tunawasaidia waweze kujiamini na kuwapa motisha ya kujifunza lugha ya Kiswahili kwa kuwazawadi mara moja moja wanaofanya vyema. Pia, tunawatuza wale wanaofanya vyema na kupiga hatua chanya katika Kiswahili*" (MK 6). Mwenzake wa Kakamega (mashambani) alidokeza; "*Kawaida tunawazawadi wanaofanya vyema na kuwahimiza wawe na mtazamo chanya kwa somo*" (MK 22). Matokeo haya yanawiana na maoni ya Oloo (2018) aliyetambua kuwa mbinu mwafaka za kufunza zinapotumika wanafunzi huhamasishwa kujifunza bali mbinu zisizo mwafaka zikizingatiwa matokeo yake ni ukosefu wa motisha upande wa wanafunzi. Pia yanalingana na maoni ya Schultz na Schultz (1987) wanaosisitiza kuwa ili tabia fulani idumu yafaa kuigwa, kurudiwarudiwa pamoja na kutuzwa la sivyo hufifia na baadaye hupotea kabisa.Nadharia ya utabia yasisitiza mazoezi na utuzaji katika somo lolotelile ili kuliimarisha hasa ushairi.

Aidha, wanafunzi waliwekwa katika makundi madogo madogo kutegemea uwezo wao na makundi mengine yanayochanganyisha wenye uwezo tofauti ili wapate kujifunza kutoka kwa wenzao. Mkuu mmoja wa idara Kisumu (mjini) alidhihirisha; "*Tunawaweka wanafunzi wetu katika makundi madogo madogo ili waweze kujiinua kimasomo*" (MK 18). Kulingana na wakuu wa idara Kakamega (mshambani); "*Sisi huwaweka katika makundi kutegemea uwezo na wakati mwingine kutumia makundi ya mchanganyiko wa uwezo kuwainua wenye uwezo wa chini*" (MK 15) na "*Kama walimu, tunawahimiza wanafunzi washirikiane katika shughuli zao za kudurusu mada za Kiswahili*" (MK 3). Madai haya yalilingana na maoni ya Kimani (2015) aliyebainisha kuwa ushirikiano ni mbinu ya kisasa yenye matokeo mazuri kwani wanafunzi wenye uwezo sawa huwekwa kwenye vikundi vidogo vidogo na hutumia mazoezi tofauti

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

kuimarisha umilisi wa lugha. Mbinu hii huimarisha uhusiano kupitia kwa kubadilishana mawazo, kusaidiana, kujibu maswali na kutiana moyo; kutupa motisha.

Walimu walijukumika kuwahusisha wataalam wa somo la Kiswahili katika ufunzaji wao. Chembilecho mkuu wa idara Kakamega (mjini); "*Wakati mwingine tunaweza kuwashirikisha wachochezi na wataalamu wengine wa lugha ya Kiswahili kutia ladha katika ufunzaji wetu; kuondoa uchovu wa kuwasikiliza walimu waliowazoea kila wakati miongoni mwa wanafunzi na kuwawezesha kumakinika zaidi masomoni wanapofunzwa na mgeni*" (MK 9). Mkuu mmoja wa idara Kisumu (mjini) alisisitiza haya; '*Kwa kuwashirikisha wachochezi/wataalamu wengine wa lugha katika ufunzaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili shuleni mwetu*" (MK 14). Maoni haya yanaingiliana na yale ya Owala (2014) kuwa mwalimu anayefunza L2 anastahili kufanya mipangilio ili wazungumzaji maalum kutoka nje ya shule waweze kuwatembelea kwa ajili ya kuwachangamsha kuhusu kazi za usoni.

Tena, walimu waliweza kuwarai wanafunzi kufanya mazoezi ya ziada huku pia wakiwapa mazoezi mengi ma kuyafuatilia kwa karibu kuhakikisha kuwa yamefanywa ili kuweza kukuza vipawa vyao katika somo. Kwa mjibu wa mkuu wa idara Kakamega (mjini); "*Walimu hufuatilia kwa karibu kuhakikisha kila kazi na mazoezi waliyopewa yamefanywa kwa umakini zaidi na kuwaelekeza vilivyo pakiwa na haja ya kufanya hivyo*" (MK 23). Kulingana na mkuu wa idara Kisumu (mashambani); "*Tunalazimika kuwarai wanafunzi wetu kufanya mazoezi ya ziada*" (MK 12). Maoni haya yanalingana na maoni ya Hunsen (1977) aliyesisitiza kuwa wanafunzi wenye mielekeo chanya kuhusu somo hutumia muda wao mwingi sana kufanya mazoezi katika somo hilo.

Muhimu zaidi ilikuwa kujitafutia muda na vipindi vya ziada kwani muda uliotengewa somo haukutosha. Walilazimika kufunza nyakati mbadala ili wanafunzi waweze kushirikishwa zaidi katika matumizi ya lugha ya Kiswahili huku wakijifunza mengi na kuweza kukamilisha (silabasi) mada zake ambazo ni pana mno kwa wakati unaofaa. Chembilecho mkuu wa idara Kakamega (mjini) alielezea; "*Sisi hulazimika kutafuta muda mbadala kuwafunza na kuwaelekeza pamoja na kuwapa mazoezi mengi ili kunoa makali yao katika somo kwa kuwa muda uliotengewa somo hautoshi tukizingatia mada zake tele zinazofunzwa na kutahiniwa*" (MK 23). Kulingana na mkuu mmoja Kisumu (mjini); "*Inambidi mwalimu kutafuta wakati wa ziada ndiposa aweze kukamilisha silabasi hasa Fasihi Andishi huhitaji muda sana*" (MK 2). Maoni haya yalioana na ya Hakielimu (2008) alivyonukuliwa na Mlay (2010) kuwa muda zaidi au vipindi vya ziada huwasaidia wanafunzi katika kuinua matokeo yao na hivyo kuboresha matokeo yao.

Mwisho, japo si katika umuhimu ni kuwashirikisha wanafunzi katika ufunzaji na ujifunzaji wao. Kulingana na wakuu wa idara Kakamega (mjini); "*Tunawapa wanafunzi nafasi ya kutathmini mbinu mbalimbali za ufunzaji na kutoa maoni yao wazi ili kutoa mwanga kwa mbinu bora zaidi zinazowawezesha kujifunza vyema zaidi. Isitoshe, walimu hujaribu sana kuwafikia wanafunzi wote na kuwahudumia kulingana na mahitaji yao japo idadi yao hutatiza sana juhudi hizi, lakini tunajaribu kadri ya uwezo wetu kama walimu*" (MK 11). Madai haya yanaingiliana na ya Owala (2014), ni muhimu kwa walimu kuwaelewa wanafunzi wao; waelewe usuli na mitazamo yao kuhusu L2 wanayojifunza.


Uchunguzi wa kimtazamo uliofanywa madarasani pamoja na mahojiano ulibainisha kuwa shule za mijini zilitumia vitabu vya ziada vya hadithi katika lugha ya Kiswahili (class readers) kukuza ujuzi wa wanafunzi wao katika lugha ya Kiswahili kuliko ilivyokuwa mashambani. Asilimia 83.3 (n=10) na 33.3 (n=4) ilidhihirisha kuwa vitabu vya hadithi hasa vya mradi wa kukuza ubunifu (MKUU) vilitumiwa katika vidato vya chini; kidato cha kwanza na cha pili kukuza na kuimarisha lugha zao mijini na mashambani mtawalia. Matokeo haya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

yanalingana na maoni ya Chacha (2016) na Ngugi (2009) waliogundua kuwa ni wazi kuwa wanafunzi ambao hawasomi vitabu vya hadithi vya kutosha hawawezi kuimudu lugha kwa ufasaha.

**Chati 5: Msaada wa Washikadau Mbalimbali**




Walimu walidhihirisha kuwa walipata misaada mbalimbali kutoka kwa washikadau mbalimbali japo kwa kiwango cha chini zaidi madhli kila kaunti ilibainisha kupa msaada kwa asilimia iliyokuwa chini ya 40. Walimu walidhihirisha wazi kuwa walipata misaada mbalimbali kutoka kwa serikali kupitia wizara ya elimu, wasimamizi wa shule na wachapishaji. Mwalimu mmoja Kakamega (mashambani) alitaja msaada wa ufadhili katika warsha; "*Mwalimu mkuu huturuhusu kuhudhuria makongamano ya Kiswahili na kutufadhili kwa hali na mali huku akitununulia vitabu na vifaa vinavyostahili katika ukuzaji wa stadi za lugha hii*" (MK 15). Mwenzake wa (mjini) akisisitiza; "*Usimamizi wa shule kupitia kwa mwalimu mkuu hufadhili makongamano ya walimu wa Kiswahili*" (MK 23). Mkuu wa idara Kisumu (mashambani) alidokeza; "*Usimamizi wa shule hutufadhili tunapohudhuria makongamano na warsha za Kiswahili.Wizara ya elimu hutupa vitabu vingi vya Kiswahili hasa vya kiada*" (MK 12). Mkuu wa idara Kakamega (mjini); "*Wachapishaji wa vitabu hutupa ushauri na vitabu vya kusoma hivyo kutuwezesha kupiga hatua katika ujuzi wa lugha ya Kiswahili*" (MK 10).Isitoshe, mkuu wa idara Kisumu (mashambani); "*Kufadhiliwa kwenda semina za kiswahili/makongamano pamoja na ufadhili wa kwenda kujifunza utahini wa Kiswahili; utahini unaoelekezwa na taasisi ya mtihani nchini, KNEC*" (MK 17). Matokeo haya yanaonyesha kuwa walimu wachache wa Kiswahili walihudhuria makongamano ya Kiswahili kutilia makali ujuzi wao mara moja tu kwa mwaka. Hali inayoonyesha udhaifu katika maandalizi ya walimu nyanjani na kumaanisha kuwa kuna changamoto kuu katika shughuli nzima ya ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwani maandilizi ya nyanjani husaidia kutekeleza ufundishaji wa mambo mapya na kuvuta kumbukumbu ya yale ambayo huenda yalisahaulika na walimu. Matokeo haya yanasawiana na maoni ya Oloo (2018) na Ogero (2012). Oloo alisema kuwa walimu wengi hawakuwahi hudhuria kozi za kuwapiga msasa wala kupata mawasiliano yoyote kuhusu shughuli za kitaaluma kama vile semina, warsha na simposia kuhusu ufundishaji wa masuala ibuka. Naye Ogero alibainisha kuwa walimu wengi hawakupata ujuzi kupitia warsha na semina mbalimbali za Kiswahili kwa kuwa walimu wakuu hawangegharamia mikutano hiyo kutokana na uhaba wa pesa shuleni.

**Msaada wa Washikadau Mbalimbali**

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

Isitoshe, matokeo haya yalionyesha kuwa uhaba wa vifaa vya kufunzia na kujifunzia husuluhishwa kwa njia moja au nyingine na wasimamizi wa shule kupitia walimu wakuu wa shule hizo pamoja, wachapishaji wa vitabu na serikali kupitia wizara ya elimu. Maoni haya yanalingana na ya Ambuko (2008) aliyesema kuwa walimu wengi walitegemea usimamizi wa shule zao kuwanunulia vifaa hivyo kwa kutumia pesa zilizotolewa na serikali. Maoni haya yanawiana na ya Wambua na wengine (2019) yaliyodhihirisha kuwa pesa zilizotolewa na serikali ni mbinu mwafaka ya kukabiliana na tatizo la uhaba wa vifaa vya kufunza na kujifunza Kiswahili. Aidha, walipokea ufadhili wa vifaa vya kufunza na kujifunza Kiswahili kutoka kwa baadhi ya wachapishaji kama vile Oxford.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Utafiti huu uligundua kuwa wanafunzi pamoja na walimu walipata shida kadhaa hali iliyoathiri kwa njia hasi ufunzaji na ujifunzaji wao.Licha ya kutambua umuhimu wa mwelekeo mseto katika ufunzaji walimu wengi hawakutumia mbinu hii kufunza kutokana na ukosefu wa vifaa na nyenzo za kufunzia, uhaba wa muda, idadi kubwa ya wanafunzi madarasani mwao, uhaba wa walimu pamoja na ukosefu wa ujuzi maalum katika mbinu mseto.Wanafunzi walihisi kuwa walimu walikuwa wakali sana hivyo kuvuruga ujifunzaji wao, ni vyema walimu wakuze uhusiano mwema kati yao na wanafunzi wao ili waweze kufurahia na kumakinika zaidi somoni. Ilibainika wazi kuwa kuna uhusiano mkuu kati ya mbinu za kufunzia na matokeo ya wanafunzi katika somo. Wanafunzi walionekana kufanya vyema walimu walipotumia mbinu za ushiriki na ugunduzi mkuu kufunzia kuliko walipotawala ufunzaji madarasani mwao. Pana haja kuu walimu waelekezwe vilivyo katika mbinu mwafaka za kufunzia, kufadhiliwa kuhudhuria warsha na makongamano ya Kiswahili ili kujipiga msasa na kujiinua kitaaluma, wanafunzi wahamasishwe kuhusu umuhimu wa somo hili, wachapishaji kuelekezwa vilivyo katika maswala yanayofunzwa katika kila kiwango na ukaguzi wa kina kufanywa ili kuondoa mambo yanayoweza kuwakanganya walimu na wanafunzi. Utafiti zaidi unaweza kufanywa katika vipengele vya Lugha na Fasihi ya Kiswahili ili kutambua changamoto zinazoshuhudiwa katika ufunzaji wao ili kuzitatua ipasaavyo.

## MAREJELEO


Aggarwal, J. C. (2001). *Principles, Methods and Techniques of Teaching.* New Delhi: Vikas Publishing House Ltd.

Akaka, L.(Haijulikani). Changamoto zinazowakabili Walimu katika Ufundishaji wa Kiswahili katika shule za Upili Nchini Kenya. *Research Article Kioo cha Lugha Juz 11.*

Alharbi, A. H. (2015). Improving Students' English Speaking Proficiency in Saudi Public Schools. *International Journal of InstructionVol. 8, No. 1 Jan 2015.*

Al Hosni, S. (2014). Speaking Difficulties Encountered by Young EFL Learners. *International Journal on Studies in English Language and Literature (IJSELL),* 2(6), 22-30.

Ambuko, B. S. (2008). Selection and use of media in teaching Kiswahili in secondary schools in Emuhaya District Kenya. *Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maseno (Haijachapishwa).*

Babusa, H. O. (2010) Uchanganuzi Linganuzi wa Mielekeo na Umilisi wa Lugha ya Kiswahili wa Wanafunzi Katika Mikoa ya Pwani na Nairobi Nchini Kenya.Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Baumgartner, L. M., Lee, M. Y., Birden, S., & Flower, D. (2003*). Adult Learning Theory: A Primer Center on Education and Training for Employment*. College of Education, The Ohio University.

Birzer. M. L.(2003). The theory of andragogy applied to police training. *Bradford, 26(1), 29.*


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

Chacha, S. (2016). *Uhusiano wa Mikakati ya Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto ya Kiswahili na Umilisi wa Kusoma Katika Shule za Msingi, Kasarani, Kaunti ya Nairobi, Kenya*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.(Haijachapishwa).

Chika, P. O. (2012). The Extent of Students' Responses in the Classroom. *International Journal of Academic Research in Business and Social Sciences, 2 (1).* www.hrmars.com/journals on 02/10/2015.

Dawning, J., Keating, T., & Bennett, K. (2005). Effective Reinforcement Techniques in Elementary Physical Education: The Key to Behavior Management. *Physical Educator, Indianapolis, 62(3), 114.*

Dewald, N. H. (1999). Web-based Library Instruction: What Is Good Pedagogy? *Information Technology and Libraries, Chicago, 18(1), 26.*

Earthman, G. I. (2004). *Prioritization of 31 Criteria for School Building*. Adequacy: American Civil Liberties Union Foundation of Maryland Assessed. <http://www.actomd.org.

Gathumbi, A.W., & Ssebbunga, C. M. (2005). *Principles and Techniques in Language Teaching; a Text for Teachers Educator, Teachers and Pre-service Educators*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Gekombe, C. M. (2015). *Factors affecting teaching and learning of Kiswahili comprehension in secondary schools in Wareng Sub-County Uasin Gishu County, Kenya* (Doctoral dissertation, Moi University).

Gudu, B. O. (2015).Teaching Speaking Skills in English Language using Classroom Activities in Secondary School Level in Eldoret Municipality, Kenya. *Journal of Education and Practice, 6(35).*

Hakielimu "Citizens for Quality basic Education and democracy in Tanzania, program Strategy and Description January 2008 to December 2011," 2008.

Hunsen, J. (1977). *International Study of Achievent in Mathematics; A Comparison of twelve Countries.* Johan Wiley and Sons.

Kang'ahi, M., Indoshi, F. C., Okwach, T. O., & Osodo, J. (2012). Teaching Styles and Learners' Achievement in Kiswahili Language in Secondary Schools. *International Journal of Academic Research in Progressive Education and Development, 1(3).* www.hrmars.com/journals on 02/10/2015

Kavoi, J. M. (2019). Mielekeo ya Wanafunzi kuhusu Ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili Katika Taasisi za Kiufundi za Kitaifa Nchini Kenya. *Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Rongo.*

Kerlinger, N. F. (1978). *Foundation of Behavioral Research*. New Delhi, Surjeet Publicatio

K.I.E. (2002). *Secondary Education Syllabus*, Volume one. Nairobi: K.I.E.

Kimani J. N.(2015). *Uhusiano wa Mbinu za Kufundisha Sarufi na Umilisi wa Mazungumzo ya Wanafunzi wa Sekondari, Kaunti ndogo ya Thika Magharibi, Kenya.* Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kitivo cha Elimu (Haijachapishwa).

Kobia, J. M., & Ndiga, T. K. (2013). The Influence of Secondary School students' Attitude towards implementation of Kiswahili Curriculum in Igembe South District, Meru County, Kenya. *International Journal of Education and Research, 1(12).*

Kolawole C.O.O. (2002). An Examination of the National Policy of Language Education in Nigeria and its Implication for the Teaching and

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538

Learning of English Language. *Ibadan Journal of Education Studies.*

Koross, R., & Murunga, F. (2017). *Mbinu za Kufundishia Kiswahili katika K21*. Eldoret, Utafiti foundation.

Liu, C. H., & Mathew, R. (2005). Vygotsky's Philosophy: Constructivism and Its Critics Examined. *International Education Journal, 6(3), 386-399.*

Lumala, P. F. M. (2007). *Towards the reader-text interactive approach to teaching imaginative texts: the case for the integrated English curriculum in Kenya* (Doctoral dissertation, University of Nottingham).

Mbito, J. K. (2013). Challenges facing teachers and students in the process of teaching and learning Kiswahili in public secondary schools in Kiambu district in Kiambu County, Kenya. *Unpublished research project submitted to Kenyatta University*.

Melly, K. J. (2019). Matumizi ya vifaa vya kisasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Sarufi:Mfano wa Shule za Upili Kaunti ndogo ya Moiben, Kenya**.** *Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kibabii (Haijachapishwa).*

Miima, F. A. (2014). *Integration of Information Communication Technologies in teaching and learning of Kiswahili language in public secondary schools in Kakamega County, Kenya*. Kenyatta University, Nairobi, Kenya

Mlay, N. (2010). *The influence of the language of instruction on students' academic performance in secondary schools: A comparative study of urban and rural schools in Arusha-Tanzania* (Master's thesis, University of Oslo).

Munawaroh, N. (2017). The Influence of Teaching Methods and Learning Environment to the students' Learning Achievement of Craft and Entrepreneurship Subjects at Vocational High School. *International Journal of Environmental and Science Education. Vol. 12 No.4. pg 665-678* .

Muruguru, S. K. P. (2000). *Students' performance in Kiswahili: A study of selected secondary Schools in Nakuru District, Kenya.* Unpublished M. Phil. Thesis. Moi University, Eldoret, Kenya.

Mutsotso, S. na Nasongo, J. (2013). The adequacy of instructional materials and physical facilities and their effects on quality of teacher preparation in emerging private primary teacher training colleges in Bungoma County, Kenya. *International Journal of Science and Research, 2(1), 403-408*

Mwakarayz (2011). *Athari za Lugha ya Kijita katika Kujifunza Kiswahili.* Tasnifu ya Uzamili (M.A. Kswahili). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa).

Ng'ong'a (2002). *An Assessment of University English Language Teacher Education in the light of Classroom needs. A case study of Maseno Unviversity.* Unpublished PhD Thesis, Maseno University.

Njagi na wengine (2014). Effectiveness of Professional Development on English and Literature teachers in selected schools in Tharaka-Nithi and Meru County, Kenya. *American International Journal of Contemporary Research Vol. 4. No. 8, 2014.*

Njoroge, F. K., & Ndirangu. M. (2018). Influence of Selected Factors on the Performance of Kiswahili Language at KCSE in Secondary Schools in Njoro Sub- County, Nakuru County, Kenya. *International Journal of Education and Research, 6(2). ISSN: 2411-5681 (www.ijern.com).*

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1538


Ngugi wa Thiongo (2009). *Remembering Africa.* East African Educational Publishers. Nairobi, Kenya.

Nwanekezi, A. U. (2006). Effects of Individualistic Learning Strategy on Students' Interest in Agricultural Science. *Journal of Technology and Education in Nigeria, 11(1).*

Odhiambo, (2012). *Taskforce on the Realignment of the Education Sector to the Constitution of Kenya 2010: Towards a Globally Competitive Quality Education for Sustainable Development.* Report of the Task Force- MOE, Kenya.

Ogero, J. O. (2012). *Institution based factors influencing students' performance in Kiswahili at KCSE in public schools in Sameta Division, Kisii County: Kenya.* Unpublished Masters Thesis Kenyatta University.

Ogott, G. O., & Odera, F.Y. (2012) Integration of Media and Technology in Teaching and Learning Kiswahili Language in Secondary Schools in Siaya County, Kenya. *International Journal of Information and Communication Technology Research, 2(10).*

Oloo, M. A. (2018). *Masuala yanayoathiri Ufunzaji na Ujifunzaji wa somo la Ufahamu katika shule za upili katika kaunti a Kisumu nchini Kenya*. Unpublished Med Thesis Chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro (MMUST)

Onyango, J. (2008). *Second Language Learning.* Unpublished module, Kenyatta University.

Opunde, S. (Haijulikani). *Mwelekeo Mseto katika Ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili.Karatasi ya utafiti.* Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro (MMUST).(Haijachapishwa).

Owala, J. A. (2014). *Mitazamo kuhusu Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kijaluo: Kifani cha shule za msingi katika kaunti ya Migori.* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Plotkin, H. (2003). We-intentionality: An essential element in understanding humanculture. Perspectives in Biology and Medicine.*Chicago, 46(2). 283.*

Roblyer, M.D. (2006). *Intergrating Educational Technology in Teaching. (Sixth Edition).*Pearson Education Limited. Edinburg Gate Harlow.www.pearsoned.co.uk.

Ruddell, R.B. (2002) *Teaching Children to read and write: Becoming an Effective Literacy teacher (Third Edition).* Boston:Allyn and Bacon.

Rutere, J. K. (2012). *Effects of teacher related factors on implementation of integrated Kiswahili curriculum in public secondary schools in Nkuene Division, Imenti South district, Kenya* (Doctoral dissertation, University of Nairobi, Kenya).

Schultz, A. & Schultz, F. (1987). A Neural Substrate of Predication and Reward. Science.275:1593-1598.

Simiyu, M.N. (2013). *Factors Affecting Academic Performance in Secondary Schools in Kenya: A case of Trans-Nzoia West District.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi (Haijachapishwa).

Tume ya Koech (1999). *Report of the Commission of Inquiry on the Education system in Kenya*. Nairobi; Government Printer Kenya.

Wambua na wengine (2019).Teaching and Learning Resources in Kiswahili in Secondary Schools. *Journal of Pedagogical Sociology and Psychology Volume 1, Issue 2, 2019 pg 64-79 www.j-psp.com*

Wanyama, P.O. (2007). Silabasi Mpya: I Wapi Tofauti? *Education Insight,* 4(2).


 | This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.